## Orodha ya kabla ya Usafiri

- ☐ Tayari nilituma **mizigo ya ziada** yangu yote. Kiwango cha mzigo na idadi ya kilo zinazoruhusiwa vyote vimeandikwa vizuri kwenye waraka wangu wa kuhifadhi nafasi ya usafiri.
- ☐ Ninao **mkoba wangu wa plastiki wa IOM** na nitaubeba kwa njia inayoonekana kama itahitajika ili kupata usaidizi wa kubadili ndege na ule wa kuwasili kwenye uwanja wa ndege.
- ☐ Nina Pasipoti yangu asilia na halali au Waraka/Laissez Passez, wa dharura wa Safari, pamoja na ule wa wale wanaonitegemea.
- ☐ Sina kitu chochote kiowevu (kikiwemo chakula kiowevu au mapambo maowevu) **krimu au vimiminika** kwenye mzigo wangu wa mkononi.
- ☐ Nilimfahamisha Mshaurinasaha wangu kuhusu **mahitaji maalum** wakati wa safari yangu (vyakula, dawa, kiti cha magurudumu, ugonjwa, n.k.).
- ☐ Kwa Wanawake Wajawazito: Ninacho cheti cha daktari kinachoniidhinisha kupanda ndege nikiwa **mwanamke mjamzito** na kinachobainisha idadi ya wiki zilizopita kwenye uja uzito wangu.
- ☐ Ninazo **dawa na matibabu** yote ninayohitaji kwenye safari yangu na cheti asilia cha daktari kwenye mkoba wangu wa mkononi.
- ☐ Dawa zote nisizohitaji wakati wa usafiri wa ndege zimehifadhiwa kwenye mzigo wangu niliotuma tayari.
- ☐ Watoto wanaosafiri Peke yao: Ninazo nyaraka zote zinazohitajika katika usafiri nikiwa **mtoto anayesafiri** pekee, ukiwemo uidhinishwaji wa mzazi wangu na ule wa mlezi wangu wa kisheria.

Jaza tu Endapo ulituma ombi na unastahili Usaidizi wa Kutangamana upya:

- ☐ Niliijaza Fomu ya Maombi ya Kutangamana upya kwenye kile kikao cha ushaurinasaha wa kabla ya usafiri.
- ☐ Nitaijaza fomu ya mkataba wa kutangamana upya pindi nifikapo kwenye uwanja wa ndege.
- ☐ Nitaihifadhi nakala asilia, hata baada ya kurudi kwangu.
- ☐ Ninaelewa kwamba maelezo ya mawasiliano ya ofisi ya IOM kwenye nchi yangu nitokako yamo kwenye Mkataba wa Kutangamana upya.

**Maoni kutoka kwa mshaurinasaha wako au msaidizi wako wa kijamii:**

SHIRIKA LA KIMATAIFA LA UHAMAJI

SHIRIKA LA KIMATAIFA LA UHAMAJI

# MWONGOZO WA USAFIRI KWA WAHAMIAJI WANAORUDI



## Kurudi kwa Hiari kutoka Ubelgiji

SWAHILI

Towards a more integrated migration policy, made possible by the AMIF

FEDERAL AGENCY FOR THE RECEPTION OF ASYLUM SEEKERS

International Organization for Migration (IOM)
Organisation internationale pour les migrations (OIM)
Internationale Organisatie voor Migratie (IOM)

## Je, unarudi katika nchi yako asilia?

**Kurudi na Kuhamia kwa Watafutaji Hifadhi ya Wakimbizi kutoka Ubelgiji**
Umetuma ombi la kurudi kwa hiari kutoka Ubelgiji kwa usaidizi wa Shirika la Kimataifa la Uhamaji (IOM). Tunafanya kila jitihada ili kukusaidia katika hatua zote za kurudi kwako.

**Tafadhali soma kipeperushi hiki kwa umakini.**


## Kurudi Leo ili Kuijenga Kesho

### Kwenye Uwanja wa ndege (Uwanja wa ndege wa kitaifa wa Brussels/Zaventem)

• Lazima uheshimu kwa umakini idadi ya mizigo unayobeba pamoja na kilo zinazoruhusiwa ili kuhakikisha kwamba unasafiri vizuri na unaepuka kuchelewa kokote kunakowezekana.

• Eneo lako la Kukutana ni katika safu ya 6, **saa 3 kabla** ya muda wa kuondoka.

• Kwenye safu ya 6, utakutana na mmoja wa Wasaidizi wa IOM kwenye Uwanja wa ndege. Ambao hutambulika kwa urahisi huvalia jaketi la bluu na kofia ya IOM.




Safu ya 6




• Mmoja wa wasaidizi wa IOM kwenye Uwanja wa ndege atawasaidia kwenye taratibu zile za kabla ya kuondoka zikiwemo kule kuandikisha mzigo, udhibiti wa ulinzi na pasipoti na, kama itawezekana, forodha.

• Msaidizi wa IOM kwenye Uwanja wa ndege ataandamana nawe hadi kwenye lango la kupandia ambapo atakupa tiketi yako ya ndege.

• Utapaswa kutumia **mkoba wa IOM** ili kuweza kutambulika kwako kwa urahisi na wafanyakazi wa IOM kwenye safari yako yote mpaka utakapofika kwenye uwanja wa ndege wa mwisho.



### Wakati Unapobadili ndege

• Kama huna ndege ya moja kwa moja, utasaidiwa na wafanyakazi wa IOM kwenye viwanja vya ndege vikubwa vya Ulaya.

• Kama mtakubaliana kabla ya kuondoka kwako, IOM itakusaidia wakati wa ubadilishaji wa ndege yako nje ya Ulaya, ikiwa inawezekana.

• Endapo unasaidiwa na IOM katika kubadili ndege ni lazima ubebe mkoba wako wa IOM. Wafanyakazi wa IOM wataweza kukutambua vizuri zaidi.

• IOM inahakikisha kwamba unaondoka kwa usalama na kwa wakati unaofaa kwa kutumia ndege inayokufaa.

• Kama ulimfahamisha mshaurinasaha wako kwamba utahitaji usaidizi maalum wa kimatibabu, IOM itaweza kuhakikisha ufuatiliaji wako mzuri na kampuni ya usafiri na hudumu za uwanja wa ndege.

• Kama utahitajika kulala njiani katika kubadili ndege, IOM inaweza kuandaa mipangilio ya malazi kwa niaba yako.





### Pindi Unapowasili

• Kama mtakubaliana mapema, IOM itakukaribisha pindi unapowasili kule uendapo na kukuhakikishia usafiri mapema hadi kule unakofikia ndani ya nchi yako ya asili. Ili kutambuliwa kwa urahisi na IOM lazima ubebe mkoba wako wa IOM.

• IOM inakusaidia kwenye taratibu zinazohitajika zikiwemo za udhibiti wa forodha na uhamiaji.

• Kama utahitaji usaidizi maalum wa kimatibabu, IOM inahakikisha ufuatilizi wako kamilifu kwenye huduma zilizopo (ambalensi na/au daktari, kwa mfano).

## Tunawatakia safari njema mnaporudi nyumbani!

**IOM Ubelgiji na Luxembourg**

Rue Montoyerstraat 40
1000 Brussels

Simu: +32 (0) 2 287 70 00
Faksi: +32 (0) 2 287 70 05
Baruapepe: IOMBrusselsREAB@iom.int
Shirika la Kimataifa la Uhamaji

